MWONGOZO WA SAFARI KWA WAGENI

Karibu

HARUSINI MIKUMI

Jumapili, 29 Novemba 2026

Mikumi Wildlife Lodge

Kwa ufupi

SIKU YA HARUSI

Sherehe inaanza	Fika kabla ya
11:00 AM	**10:00** AM

SHUTTLE NI BURE

Kwa wageni wote, tarehe 29 tu: kutoka Morogoro kwenda Mikumi asubuhi, na kurudi Morogoro jioni.

Jisajili kabla ya 15 Novemba 2026

TAARIFA KUHUSU MALAZI

Kwa wageni watakaopenda kulala Morogoro au Mikumi Wildlife Lodge, gharama za malazi ni juu ya mgeni mwalikwa.

Muhimu: Ada ya kuingia hifadhi (TANAPA) hulipwa kwa **control number**, si fedha taslimu. Beba kitambulisho chako.



Safari yako

JINSI YA KUFIKA

DAR ES SALAAM

Stesheni ya SGR

Treni ya SGR · inaondoka 6:00 AM

TAKRIBAN SAA 2

MOROGORO

Stesheni ya SGR (7:45 AM) au Morena Hotel (8:00 AM)

Shuttle ya bure · tarehe 29 tu

TAKRIBAN SAA 2

MIKUMI WILDLIFE LODGE

Umefika! Sherehe inaanza 11:00 AM.

Kurudi ni njia ileile: shuttle 5:30 PM, treni 8:30 PM.

Jumapili, 29 Novemba

Ratiba ya siku

KWENDA

6:00 AM	Treni ya SGR inaondoka Dar es Salaam
7:45 AM	Shuttle inachukua wageni Stesheni ya SGR Morogoro
8:00 AM	Shuttle inachukua wageni Morena Hotel
10:00 AM	Kufika Mikumi Wildlife Lodge
11:00 AM	**Sherehe inaanza**

KURUDI

5:30 PM	**Shuttle inaondoka Mikumi kwenda Morena Hotel na Stesheni ya SGR Morogoro**
7:30 PM	Kufika Morogoro (takriban)
8:30 PM	Treni ya SGR inaondoka Morogoro kurudi Dar es Salaam

Shuttle inaondoka **5:30 PM kamili**. Magari hayaruhusiwi kutoka hifadhini baada ya 6:00 PM.



Gharama kwa mtu mmoja

Chagua mpango wako

1 Siku moja kwa treni

Safiri na urudi tarehe 29. Shuttle ni bure.

Kuanzia TSh 79,000

2 Lala Morogoro

Fika tarehe 28 na ulale Morogoro mahali utakapopendelea. Kesho yake, tukutane Morena Hotel 8:00 AM kupanda shuttle.

Kuanzia TSh 134,000

3 Lala Mikumi Wildlife Lodge

Fika tarehe 28 kwa usafiri wako, ulale mahali pa sherehe.

Takriban TSh 305,500

Bila gharama za gari



Mpango 1
Siku moja kwa treni

Treni Dar → Morogoro, 6:00 AM	22,500 – 45,500
Treni Morogoro → Dar, 8:30 PM	50,500 – 63,500
Shuttle Morogoro ↔ Mikumi	Bure
TANAPA, kuingia hifadhini	6,000
Jumla (TSh)	**79,000 – 115,000**

* * *

Mpango 2
Lala Morogoro

Mfano: Morena Hotel, Morogoro · TSh 110,000 kwa chumba

Treni Dar → Morogoro, tarehe 28 Treni yoyote; tarajia bei kama za treni ya 6:00 AM	22,500 – 45,500
Malazi Morena Hotel, usiku 1 55,000 kwa mtu ikiwa chumba kimoja kinashirikiwa na watu 2; 110,000 ukilala peke yako	55,000 – 110,000
Shuttle, 8:00 AM Morena Hotel	Bure
Treni Morogoro → Dar, 8:30 PM	50,500 – 63,500
TANAPA, kuingia hifadhini	6,000
Jumla (TSh)	**134,000 – 225,000**

Morena Hotel ni pendekezo letu tu. Unakaribishwa kulala popote utakapopendelea Morogoro; tukutane Morena Hotel saa **8:00 AM** kupanda shuttle.



Mpango 3
Lala Mikumi Wildlife Lodge

$110 kwa mtu, pamoja na malazi na milo 3

Malazi na milo 3, usiku 1	291,500 ($110)
TANAPA, kuingia hifadhini (mara moja tu)	6,000
TANAPA, kulala hifadhini ($3 kwa mtu)	8,000
Jumla kwa mtu (TSh)	**305,500**

Haijajumuishwa: kibali cha gari binafsi (TSh 30,000 kwa gari) na mafuta.

Bei ya punguzo

Bei ya $110 ni punguzo maalum kwa wageni wa harusi.

Thibitisha nasi kabla ya 24 Oktoba 2026

Baada ya hapo, chumba kinaweza kuwa $340 kwa mtu mmoja (≈ TSh 901,000) au $454 kwa chumba cha watu 2 (≈ TSh 1,203,000).

Unakuja kwa gari lako tarehe 29 tu? Utalipa TSh 30,000 kwa gari na TSh 6,000 kwa kila mtu.

• • •

Safari ya treni

Nauli ya SGR

Kwa mtu mmoja, safari moja

TRENI	ECONOMY	BUSINESS	ROYAL
Dar → Morogoro 6:00 AM	22,500	35,500	45,500
Morogoro → Dar 8:30 PM	—	50,500	63,500

Treni ya 8:30 PM haina daraja la Economy. Bei zinaweza kubadilika; thibitisha kabla ya kukata tiketi.

• • •

Hifadhi ya Mikumi

Ada za TANAPA

Hulipwa kwa control number, si fedha taslimu

Kuingia hifadhini Kwa mtu, mara moja tu	TSh 6,000
Kulala hifadhini Kwa mtu, kwa usiku; wanaolala Mikumi Wildlife Lodge tu	$3 ≈ TSh 8,000
Gari binafsi Kwa gari	TSh 30,000

Dola zimebadilishwa kwa takriban TSh 2,650 kwa $1.

• • •

Kabla ya safari

Kumbuka

Beba **kitambulisho**, kwa treni na kuingia hifadhini.

Kujisajili kwa shuttle na maswali kuhusu safari: utapata maelezo kwenye **group la WhatsApp**.

• • •

Tunawasubiri kwa furaha

MIKUMI · 29.11.2026